



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA MANISPAA YA SONGEA**



**KIZIDUO CHA MUHTASARI WA KIKAO CHA MENEJIMENTI MWEZI  
JUNI KILICHOFANYIKA TAREHE 13/10/2021 KATIKA UKUMBI WA MANISPAA YA  
SONGEA.**

**KUMB.NA.SO/MC/CMT/100/2021 - MAHUDHURIO**

1. Andambike B. Kyomo- Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa - Mwenyekiti
2. Buaruan S. Mapunda- Kaimu Mkuu wa Idara ya Utumishi na Utawala – Katibu
3. Rozina Chuwa - Mkuu wa Idara ya Mifugo na Uvuvi wa Manispaa
4. Joel Mairo - Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani wa Manispaa
5. Amina Pilly - Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Teknolojia, Habari na Mawasiliano wa Manispaa
6. Zawadi Nguaro - Mkuu wa Idara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika wa Manispaa
7. Emmanuel Mgaya - Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara wa Manispaa.
8. Aman Mmassi - Kaimu Mkuu wa Idara ya Usafi na Mazingira wa Manispaa
9. Caroline M. Bernard - Kaimu Mkuu wa Idara ya Ujenzi wa Manispaa
10. Alex M. Mshana - Kaimu Mkuu wa Idara ya Ardhi na Mipango Mji
11. Theresia Mbawala - Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Sheria wa Manispaa
12. Clement M. Sanawa - Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Ugavi na Manunuzi wa Manispaa
13. Martin C. Mtani - Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii wa Manispaa
14. Marilyn Simbo - Kaimu Mkuu wa Idara ya Afya wa Manispaa
15. Godfrey Luhimbo - Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Nyuki wa Manispaa
16. Furaha Mwangakala - Afisa Biashara wa Manispaa
17. Mustapha Matili - Mhasibu wa Mapato

**SEKRETARIETI**

1. John E. Puppa

**KUMB.NA.SO/MC/CMT/101/2021 – KUFUNGUA KIKAO.**

Kaimu Mkuu wa Idara ya Utumishi na Utawala wa Manispaa ambaye alikuwa (Katibu) alimkaribisha Mwenyekiti kufungua kikao baada ya akidi kukamilika. Kisha Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa (Mwenyekiti) alifungua kikao saa 11.50 asubuhi.

**KUMB. NA. SO/MC/CMT/102/2021 - KUIDHINISHA AGENDA**

Jumla ya dondoo kumi na tano (15) ziliwasilishwa na kuidhinishwa na wajumbe zijadiliwe kwenye kikao hiki ambazo zilikuwa:-

1. Kufungua Kikao.
2. Kuidhinisha Agenda.
3. Kusoma na kuthibitisha mihtasari ya vikao vya Menejimenti vilivyofanyika tarehe 24/08/2021.



4. Yatokanayo na kikao cha Menejimenti kilichofanyika tarehe 24/08/2021.
5. Kupitia muhtasari na yatokanayo na Kikao cha Kamati ya Fedha na Utawala kilichofanyika tarehe 25/08/2021.
6. Taarifa ya mapato na matumizi ya Septemba Agosti , 2021.
7. Maombi ya kuanzisha fedha ya Matumizi Matumizi madogo madogo Tsh. 10,000,000
8. Mapendekezo ya kuboresha Matumizi ya bustani ya Manispaa
9. Taarifa ya maeneo yanayokusudiwa kutangazwa kuwa maeneo ya urasimishaji katika Manispaa
10. Maombi mbalimbali ya Ardhi
  - 9.1 Ombi la Mchoro No. 09/SOG/189/092020
  - 9.2 Ombi la Mchoro No 09/SOG/217/102020
11. Maombi ya kupunguziwa kodi ya pango la kibanda na 281 kilichopo Soko Kuu
12. Maombi ya kupunguziwa kodi ya pango la vibanda vilivyopo Stendi kuu ya Tanga
13. Taarifa ya Uteuzi wa wajumbe wa Bodi ya Zabuni
14. Taarifa kuhusu kuwasilisha Miradi inayotekelezwa katika Manispaa
15. Uwasilishaji wa mapokezi ya fedha za UVIKO19 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya mendeleo
16. Kufunga Kikao

**KUMB. NA. SO/MC/KFU/115/2021- UWASILISHAJI WA MAPOKEZI YA FEDHA ZA UVIKO19 KWA AJILI YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MENDELEO**

Taarifa ya fedha za UVIKO19 Tsh 660,000,000 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi y Mendeleo iliwasili kwenye kikao kwa mchanganuo ufuatao.

Tsh 520,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba 26 vya madarasa ya shule za sekondari.

Tsh 80,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa bweni moja la wanafunzi wa shule za msingi wenye uhitaji maalum

Tsh 60,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vitatu vya madarasa katika shule za msingi.

Jumla ya fedha yote iliyopokelewa ni Tsh 660,000,000

Wajumbe walipokea taarifa na kuiadili hatimaye walipanga mikakati ya kufanya utekelezaji wa miradi hiyo haraka.

**KUMB. NA. SO/MC/KFU/116/2021-** Mwenyekiti aliwashukuru Wajumbe na kuwasisitiza kwenda kufanyia kazi makubaliano ya kikao, kisha alifunga kikao saa 4.57 mchana

UMETHIBITISHWA NA:-

  
.....  
Mwenyekiti

  
.....  
Katibu

Tarehe: 13/10/2021